TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)
(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)
S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamiii:instagram/fb, taro.tz
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo,
Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam
"Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote"
TARO
TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

Ref.No: Taro /P/2022/ A07 **: Swahili Version:** Date: 9th March 2022

## UFAFANUZI KWA WASIOELEWA SHUGHULI ZA TARO NA KUANZA KUJENGA HOJA MBALIMBALI

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** au kwa lugha ya Kiswahili **"TAASISI YA HAKI ZA WASANII"** ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiriwa na sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali iitwayo **"Non Governmental Organization Act.No.24. of 2002"**, Mnamo tarehe **26/11/2021**. Lengo kuu la **TARO** ni kuiwezesha jamii ya kitanzania kushiriki kikamilifu katika kupambana na umasikini kwa kutumia sanaa na fasihi. Katika kuakikisha inafanikiwa kwenye lengo lake kuu tajwa, moja ya shughuli za TARO ni kusaidia kulinda haki na maslahi ya wasanii wote kuhusiana na kazi zao za sanaa.

Tangu TARO tuanze kutoa matamko ya kulaani vitendo vya COSOTA na BASATA kuvunja sheria, tunafurahi kupata mapokeo mazuri kwa wadau mbalimbali wa sanaa na utamaduni. Lakini imeonekana kuwa kuna baadhi ya watu wachache kuonyesha kutoelewa mwenendo mzima wa shughuli za TARO. Tunaheshimu maoni ya watu wote ila tuko huru kuchambua na kukubaliana na baadhi ya maoni

Baadhi ya watu wasiotuelewa hawakuweza kuonyesha uhalali wa kisheria wa COSOTA na BASATA kuvunja sheria, kanuni, sera na miongozo ya serikali iliyowekwa kuongoza utendaji wa taasisi hizo. Bali walijikita katika kukaa mbali na hoja za msingi za kisheria za TARO ambazo ni uvunjifu wa sheria, kanuni, sera na miongozo ya serikali unaofanywa na COSOTA na BASATA.

Katika jitihada zao waliweka nguvu kubwa katika kubadilisha muelekeo wa TARO na kutengeneza hoja ndogo ndogo zisizokuwa na misingi ya kisheria wala mahusiano na haki na maslahi ya wasanii. *Wengine walienda mbali na kuitaka TARO isisimamie sheria, kanuni, sera na miongozo ya serikali inayoongoza utendaji wa taasisi za umma (COSOTA na BASATA)*

Msingi mkuu wa matamko yote ya TARO ni ulinganifu baina ya utendaji wa COSOTA - BASATA na maelekezo ya sheria, kanuni, sera na miongozo ya serikali katika utendaji wao. TARO tunaheshimu utu, thamani ya utu na haki za binadamu. Hatujihusishi na majungu,

propaganda wala matamko ya kisiasa. Shughuli za TARO zimejikita katika misingi ya sheria (Strictly law)

Maoni ya watu wasiotuelewa yalihusisha uongezwaji wa maneno ambayo hayakuandikwa katika matamko ya TARO. Matamko yote ya TARO yanapatikana kwenye mitandao yetu ya kijamii, **instagram** @taro.tz @sherianasanaa , **tweeter** @taro.tz , **facebook** @sheria na sanaa-TAROTZ. Maneno hayo yalioyoongezwa yameorodheshwa hapo chini kama ifuatavyo:-

i. Wasanii ni lazima wapeleke habari za mafanikio ya shughuli zao BASATA.
ii. Kuna wasanii wameleta malalamiko TARO. Ifahamike kuwa TARO tunahaki ya kisheria kuzungumzia jambo lolote linalokandamiza haki na maslahi ya wasanii hata bila kuambiwa na msanii yoyote, kama ilivyo kwenye Asasi zinazoshughulikia haki za watoto, ili mradi tu jambo hilo liwe linatendeteka
iii. Kutaka taasisi ya umma (BASATA) kuwasifia wasaniii.Tulichokisema ni kwamba BASATA ni lazima kutambua na kuenzi wasanii wenye vipaji maalumu vinavyohusiana na utamaduni kama sera ya utamaduni(1999) inavyoeleza na sio kusifia wasanii.

Pia hoja mbalimbali ziliwasilishwa na watu hao wasiotuelewa kama zilivyoorodheshwa hapo chini:-

1. TARO hatujaonyesha kama kuna sheria zimevunjwa na madhara yake katika matamko yetu.
2. TARO ingekaa na COSOTA kama mdau kujadili na kutafuta ufumbuzi juu ya changamoto husika
3. TARO inalalamika kwa niaba ya msanii x yaani wakili wa msanii x
4. COSOTA wako sawa kutokufuata sheria zao zinavyowaelekeza kama msanii hajaridhika na huduma zao aende mahakamani.
5. BASATA ikisajiri wasanii inapotokea matukio itafeli.
6. TARO wanalalamika bila kushauri ufumbuzi wa changamoto wanazoziorodhesha pia ni wazodoaji tu

**MAJIBU YA HOJA ZILIZOWASILISHWA NA WATU WASIOTUELEWA**

1. *TARO hatujaonyesha kama kuna sheria zimevunjwa na madhara yake katika matamko yetu.*

Kulingana na hoja hiyo ya kwanza TARO, tunajibu kuwa tunaomba watu msiotuelewa msome kwa umakini matamko yetu, mtaona vifungu vya sheria vilivyovunjwa vimeorodheshwa, pia madhara ya uvunjifu huo yameoanishwa katika kila hitimisho la tamko.

2. *TARO ingekaa na COSOTA kama mdau kujadili na kutafuta ufumbuzi juu ya changamoto husika*

Kulingana na hoja ya pili, COSOTA ilishawahi kuandikiwa barua juu ya kufuata utaratibu wake kisheria na mmoja wa walalamikaji wa uvunjifu wa hakimiliki lakini walipuuza. Pia swala la taasisi ya serikali kufuata sheria, kanuni, sera na miongozo ya serikali, si swala la kujadiliana na

kutafuta ufumbuzi, bali ni swala la lazima. *Kama taasisi ya serikali imeshindwa kufuata sheria zake, itafuata hekima za viongozi wa taasisi zisizo za kiserikali katika mijadala?*

3. *TARO inalalamika kwa niaba ya msanii x yaani wakili wa msanii x*

Kulingana na hoja ya tatu, TARO tumesajiliwa kufanya kazi zetu kwa niaba ya wasanii wote, kwa hivyo sio tatizo kushughulikia haki na maslahi ya msanii yoyote au kumuongelea msanii yoyote.

4. *COSOTA wako sawa kutofuata sheria zao zinavyowaelekeza kama msanii hajaridhika na huduma zao aende mahakamani.*

Kulingana na hoja ya nne, TARO tunasikitika kwa uelewa mdogo sana wa sheria wa mtoa hoja. Kama COSOTA haina haja ya kufuata sheria,kanuni, sera na miongozo yake basi hakuna maana nzima ya uwepo wa COSOTA na mambo yote yangefanyika mahakamani. Sheria kuipa majukumu COSOTA, imeona umuhimu wa COSOTA katika kutekeleza majukumu hayo.

5. *BASATA ikisajiri wasanii inapotokea matukio itafeli.*

Kulingana na hoja ya tano, mtoa hoja hakuelezea BASATA itafelije. Kulingana na sera ya utamaduni (1999) katika kipengele 4.1.1, ni jukumu la BASATA kuhamasisha wasanii kushiriki katika maonyesho na matamasha mbalimbali. Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa 2018 zimetungwa kutekeleza sheria ya Sanaa (Nation Art Act.No.23 of 1984) na sera ya Utamaduni 1999. Kumnyima msanii kushiriki katika tamasha au maonyesho kisa hajasajiliwa wakati kuna nafasi ya kumsajili kisha akashiriki sio muelekeo wa serikali kwa mujibu wa sera. Zinapotokea fursa ndio nafasi nzuri ya kuhamasisha wasanii kujisajili kwa wingi.

6. *TARO wanalalamika bila kushauri ufumbuzi wa changamoto wanazoziorodhesha pia ni wazodoaji tu*

Kulingana na hoja ya tano, TARO hatujawahi kulalamika bali tunaziambia taasisi hizo husika kufuata sheria ambalo ni jambo la lazima. Lakini pia hata kama tungekua tunalalamika, kuilalamikia taasisi ya serikali si jambo baya kama linavyotafsiriwa na wengi kiupotoshaji. Serikali pia inatambua umuhimu wa malalamiko ndio maana imeweka miongozo. Rejea kipengele cha 1.5, Sura ya Kwanza ya **Mwongozo wa Ushughulikiaji wa Malalamiko ya wananchi katika utumishi wa Umma, Desemba 2012**, kinatafsiri kuwa malalamiko "*ni kitendo cha mteja, kikundi cha watu au taasisi kuonyesha hali ya kutoridhishwa na huduma iliyotolewa na Taasisi hivyo kuamua kutoa taarifa ya kutoridhika kwa mtumishi aliyehusika au Taasisi yake kwa matarajio kuwa marekebisho yatafanywa"*

Kuhusu ufumbuzi wa changamoto tayari TARO tumekwisha waeleza COSOTA na BASATA kuwa wafuate sheria,kanuni,sera na miongozo yao iliyowekwa na serikali. Kutokufuata sheria ni changamoto kubwa inayozuia upatikanaji wa HAKI KWA WASANII.

**HITIMISHO**

Matamko yote ya TARO yameandaliwa yakiwa yamejikita katika misingi ya sheria, kwa kuheshimu utu, heshima ya utu na haki za binadamu. Angalizo kwa wanaoamua kutoa maoni yao juu ya matamko yetu. Ikiwa watatoa maoni yao kwa kunukuu vibaya na kujikuta wanashambulia nafasi za kibiashara za watu binafsi (wasanii), heshima zao, mahusiano na taasisi yoyote, watawajibika kisheria wao binafsi bila kuihusisha TARO. Matamko ya TARO ni nyaraka za kisheria zilizobeba haki na maslahi ya watu, umakini wa hali ya juu unahitajika kuzitumia. Tunashauri watu wote wasome matamko yetu taratibu na kwa umakini bila kuhusisha mihemko, kwani matamko yetu yote yana nia njema kwa wasanii na nchi kwa ujumla. Pia kwa siku zijazo, TARO hatutajiingiza sana kujibu hoja zisizokuwa na misingi ya kisheria. TARO hatujihusishi na udaku, majungu, propaganda wala matamko ya kisiasa.

*Mnamo tarehe 8 Mwezi Machi 2022, TARO tuliungana na wanawake wote nchi katika kusheherekea siku ya wanawake duniani. Tunampongeza sana Mheshimiwa, **Raisi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu** kwa kuzidi kuimarisha misingi ya **Haki na Amani** nchini.*

ASANTENI
MUNGU AIBARIKI TANZANIA
MUNGU ATUBARIKI WATANZANIA
(Kazi iendelee)

Wako katika kujenga Taifa

**Mkurugenzi Mkuu wa Utawala**
**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**